

**OR-TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**  
**SHULE YA SEKONDARI KASOKOLA**

S . L . P 551.

10/12/2022

Simu: 0622361956/0763093334 /0766757020

UnapojibuTafadhali taja:

KUMB.NA.KTV/MMC/KSS/KDT I-6/1/2022

MZAZI WA .....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KASOKOLA ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA MKOA WA KATAVI -2022**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza (I) mwaka **2022** Katika shule ya sekondari Kasokola,**hongera.**

Shule ya sekondari Kasokola ipo umbali wa kilomita kumi na mbili (12) kutoka Mjini Mpanda pembezoni mwa barabara iendayo **UGALA**. Usafiri wa Bodaboda na bajaji unapatikana mjini nauli ni shilingi elfu tano (5000/=). Ukipanda bajaji toka mjini mpaka Nyerere mwisho wa bajaji ni Tsh.500. Na kutoka Nyerere mwisho wa bajaji ni Tsh.2000/= kwa pikipiki kuja shuleni.

Muhula wa masomo unanza tarehe **17/1/2022** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **17/1/2022** kwa wanafunzi wa kutwa na wale wa Hostel (Daharia) Mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/1/2022**. **Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti.**

**Mzazi/mlezi** wa mwanafunzi unatakiwa kusoma na kujaza fomu ya **AFYA** kwa kumpima mwanao kwenye Hospitali au Kituo cha Afya cha serikali, ili kuepuka usumbufu siku za baadaye.

**“Elimu,Nidhamu na Maendeleo” Ndiyo kauli mbiu ya Shule yetu.**

Nakutakia safari njema ujapo Shule ya Sekondari Kasokola. **KARIBU.**

.....  
**MPOKI P. MWAIFUGE**  
**MKUU WA SHULE**  
**SHULE YA SEKONDARI KASOKOLA**

**-01-**

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa na utoro wa rejareja, kulala nje ya shule bila ruhusa kwa wale wanaokaa DAHARIA/hosteli
3. Kugoma adhabu na kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana au kupiga, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
6. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
7. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuo au kuolewa.
8. Kusababisha, Kupata ujauzito au kutoa mimba.
9. Kushiriki katika uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
10. Kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
11. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi popote.
12. Kudharau Wimbo na Bendera ya taifa.
13. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
14. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi kama Dawati, madirisha, milango, mfumo wa umeme nk.
15. Kutoka nje ya mipaka ya shule.

## **KANUNI ZA SHULE**

### **a. HESHIMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati ya Wanafunzi, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali safi kila wakati, kutofuga ndefu na unatakiwa kuvaa mavazi ya heshima.
7. Mwanafunzi anatakiwa kutii wito kwa haraka.
8. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa "coat of Arm", wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma. Kwa wale wa hostel(Daharia) ni wakati wa chakula.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na kusimama unapouliza na kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote unapokuwa darasani, usitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.

14. Kuheshimu na kukubali tofauti za kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.

**15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vifuatavyo shuleni **SIMU au KIFAA CHOCHOTE CHA UMEME, Pasi ya umeme "Heater", KAMERA, VYAKULA** vya aina yoyote ambavyo havikuagizwa.**

**b. MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo na muda wa ziada kwa siku 395.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria baraza la shule na ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa na mikutano ya madarasa.

**c. MAANDALIZI YA JIONI**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalizi ya jioni kwa watakaoishi BWENI kuanzia Jumatatu jumapili saa 1.00 hadi saa 4.00 usiku na alfajili ni saa 10:00 hadi 11:30. Aidha maandalizi ya masomo muda wa ziada ni kuanzia saa 10:00-11:30 jioni. **Mwanafunzi harushusiwi kukaa au kulala bwenini muda huu ukipatikana adhabu itatolewadhidi yako.**
2. Ili kufanikisha maandalizi ya jioni, Ofisi ya taaluma itakuwa inatoa kazi toka kwa walimu wazalendo na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa na kusahihishwa.
3. Walimu wa taaluma, zamu na wengine watakuwa wanasimamia maandalizi ya jioni kikamilifu.

**d. MAENDELEO YA MWANAFUZI KITAALUMA NA TABIA**

Shule hutuma taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila muhula, tafadhali mzazi/mlezi hakikisha unaipata na kumshauri mwanao kuhusu maendeleo yake.

**e. KUWAHI**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda wakati wowote.
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku au kuagizwa.
3. Kufika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kufuatana na muhuala husika.

**f. SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

1. Masomo darasani na masomo ya ziada kadri ilivyo amuliwa
2. Kutoka nje ya shule Kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini kwa wale waishio shuleni.
5. Kwenda kwenye maandamano ya shughuli za Kitaifa , Mkoa, Halmashauri na Kata.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo kwa waishio hosteli.
7. Kazi za mikono (vazi la kazi kwa wote ni T-Shirt za shule).
8. Michezo ,aje na bukta jezi ya **CHESI**.

**NB:** Mwanafunzi wa Daharia(Hostel)haruhusiwi **kuja na nguo za nyumbani** nje ya zile ulizoagizwa na shule, **kuvaa kofia, mizura, nguo fupi zenye mipasuo, kufuga kucha, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa heleni, mikufu, bangili, nguo za kubana, viatu vyenye visigino virefu, mapambo mengine yoyote akiwa shuleni na nje ya mazingira ya shule.**

#### **g. MIPAKA YA SHULE**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mwalimu.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:
  - i. Ofisi ya walimu (staffroom).
  - ii. Ofisi za shule.
  - iii. Maabara.
  - iv. Jikoni.
  - v. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
  - vi. Hostel kwa wale wasiokaa hostel

#### **h. UGONJWA**

1. Tafadhali mzazi/mlezi unatakiwa kufanya **uchunguzi wa kina wa Afya ya mwanao kabla hajaripoti** shuleni na wakati wa likizo ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
2. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matroni wa shule, mwalimu mlezi n.k. mwanafunzi harusiwi kutunza dawa yoyote Hostel. Dawa zote zitunzwe kwa mwalimu wa malezi wa shule(matron).
3. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika Daharia ya shule endapo anatumia dawa na mzazi atajulishwa kama hakutakuwa na madiliko kiafya (Kwa wale watakaokaa hostel ).
4. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au Matron wa shule, mara afikapo shuleni akiwa na viambata kuthibitisha tatizo hilo.
5. Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wanafunzi wagonjwa.

#### **ANGALIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Mwanafunzi harusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k.
3. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita eneo lisilo na njia maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka na kuziacha bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.

#### **C. MAVAZI PAMOJA NA SARE.**

1. Sketi ndefu mbili (02) urefu wa cm15 kutoka kwenye unyayo zitolewe isiyobana mwili na yenye malinda za kawaida rangi kijani- jeshi. Kwa wavulana suruali iwe pana na yenye mkunjo (turn-up) mguuni, rangi kijani- jeshi. (**unaweza kupata hapa shuleni kwa 12,000/= sketi na 13,000/= kwa suruali**)
2. Mashati mawili meupe mikono mifupi kwa WAV na WAS.
3. Rangi ya hijabu ni nyeupe kwa ajili ya darasani na nje,ziwe na urefu wa **kufunika mabega tu na zisiwe na urembo.**
4. **T-shirt rangi ya Orange**(Chungwa) YENYE nembo ya shule ni sehemu ya sare zetu( Inapatikana shuleni Tsh 13,000/= tu)
5. Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi kwa wavulana na soksi nyeusi jozi mbili (02) nzito zisizo na maua. Kwa wasichana viatu vyeusi vya ngozi vyenye mkanda mmoja na soksi nyeupe nzito.
6. **Sweta moja au mawili** rangi ya kijani jeshi (Inapatikana shuleni kwa Tsh 12,000/= tu)
7. Nguo za kushindia (shamba dress) zinatakiwa mbili (02) ziwe ndefu,ziache sentimeta 15 kutoka kwenye magoti kwenda chini, rangi ya kijani- jeshi , mshono wa solo. Kanga mbili au vitenge viwili na taulo kwa waishio hostel.

8. Mashuka mawili rangi ya bluu na pink moja moja(01) la kutandika lisilo taliziwa maua na shuka nzito la kujifunika rangi yoyote.
9. Chandarua- rangi KIJANI.

#### **VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

1. Dafutari kubwa (Counter book) 9
2. Daftari ndogo TANO 5
3. Mkebe 01, Rula 01, biki 4 na kalamu za risasi 4
4. **RIMU MOJA (1). Tumeagiza rimu moja kwa kila mwanafunzi kwa sababu shule inatarajia kuwa na mazoezi ya mara kwa mara ili kuinua ufaulu kama mkakati wa shule.**

#### **VIFAA VYA USAFI**

##### **Msichana**

Jembe 01  
Ndoo 01

##### **Mvulana**

Jembe 01  
Kwanja 01

**MUHIMU:** Nimategemeo yangu kwamba kila mwanafunzi atazingatia sheria , taratibu na kanuni za shule, pia atakuja na vifaa vingine vyote kama ilivyoagizwa kwenye fomu hii.  
**Kitambaa cha sketi na suruali vinapatikana shuleni kwa bei Tsh 5,000/= kwa mita moja,** Tafadhali usinunue kitambaa nje ya shule au kwa kumwangalia mwanafunzi wa mwaka jana amevaa kitambaa cha aina gani kuepuka muingiliano wa rangi ya sare yetu

#### **SIKU YA KURIPOTI KILA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA AJE NA MZAZI/ MLEZI, ATAKAYEKUJA PEKEYAKE HATAPOKELEWA**

Karibu Kasokola kwa elimu, nidhamu na Maendeleo bora.

**MPOKI P. MWAIFUGE**

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI KASOKOLA.**

**Kwa kuwa daharia(hostel) haiendeshwi na serikali na hakuna fedha inayotengwa kwaajili ya chakula,ukarabati,tahadhali na malipo kwa mpishi, mzazi atakaye mlete mtoto kuishi hostel, atatakiwa kutoa michango kama ifuatavyo:**

**A. MICHANGO YA KAWAIDA**

- i.TSh 34,000/= kwa ajili ya malipo ya mpishi na huduma ya hostel kwa mwaka.
- ii.Unga kg 100 kwa mwaka. Kg 50 kwa mhula wa kwanza na kg 50 mhula wa pili, unashauriwa kununua **sembe** ukizingatia muda wa kuharibika(Expiry Date).
- iii.Mchele kg 40 kwa mwaka. kg 20 kwa muhula kwanza na 20 kwa muhula wa pili.
- iv.Mahrage kg 40 kwa mwaka. kg 20 kwa mhula wa kwanza na kg 20 kwa muhula wa pili.
- v.Kande kg 20 kwa mwaka. kg 10 kwa mhula wa wa kwanza na kg 10 kwa muhula wa pili.
- vi.Mafuta lita 10 kwa mwaka. Lita 5 kwa mhula wa kwanza na Lita 5 kwa muhula wa pili.
- vii.Chumvi paketi 10 kwa mwaka. Paketi 5 kwa mhula wa kwanza na paketi 5 muhula wa pili
- viii.Vitnguu sado 2 kwa mwaka. Sado 1 kwa mhula wa kwanza na sodo kwa muhula wa pili.
- ix.Dagaa sado 2 kwa mwaka. sado kwa mhula wa kwanza sado kwa muhula wa pili.
- x.Tsh.9,000/=kwaajili ya ununuzi wa vyombo Kwa wale ambao ni mara ya kwanza kuja hostel.

**B. SARE/ MAVAZI YA WATAKAOKAA DAHARIA/HOSTEL**

- i.Ttrack suit rangi ya Dark Bluu,soksi ndefu na kofia aina ya mzura (kwaajili ya kujikinga na mbu waka wa masomo ya usiku)
- ii.Shamba dress rangi ya kijani jeshi mshono wa solo iache cm 15 toka chini.
- iii. Kandambili jozi moja

**C. VIFAA VINGINE**

- iv. Shuka mbili Bluu na Pink za kutandika na moja nzito ya kujifunika.
- v. Tracker 1
- vi. Godoro 1- Futi 2 ½ kwa 6
- vii. Chandarua (Net) Moja 1
- viii. Ndoo lita kumi (10) Mbili 2
- ix. Fagio laini 1, ngumu 1 na ya kudekia (mopper) 1
- x. Sahani 1 na Bakuli1, Kijiko 1 na kikombe 1.

**NB: MWANAFUNZI WA DAHARIA (HOSTEL) HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI (zisizoagizwa)**

Karibu Kasokola kwa elimu, nidhamu na Maendeleo bora

.....  
**MPOKI P. MWAIFUGE**  
**MKUU WA SHULE**  
**SHULE YA SEKONDARI KASOKOLA.**

